



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA



TAREHE 27.10.2021

---

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela anapenda kuwatangazia nafasi za kazi za mkataba wa mwaka mmoja (01) kwa wataanzania wenye sifa kama ifuatavyo:

### 1. Mhandisi Ujenzi Daraja la II ( Nafasi 1)

Ngazi ya Mshahara TGS E

Kituo cha kazi: Halmashauri ya Wilaya ya Kyela

#### Sifa za Mwombaji

- Awe Mtanzania mwenye umri kuanzia miaka 18 hadi 45,
- Awe na Elimu ya Shahada/Stashahada ya juu ya Uhandisi kutoka vyuo vikuu vinavyotambuliwa na Serikali katika mojawapo ya fani ya uhandisi wa majengo, madaraja au barabara
- Awe na uzoefu usiopungua miaka mitatu (03) katika fani ya uhandisi wa majengo/madaraja/barabara.
- Maombi yaambatanishwe na picha mbili (2) passportisize.
- Maombi yaambatanishwe na cheti cha kuzaliwa cha mwombaji.

## **Majukumu**

- Kufanya ukaguzi wa barabara, madaraja na majengo mbalimbali ya Halmashauri
- Kuchunguza vyanzo vya ajali barabarani.
- Kufuatilia utekelezaji wa Sheria na Kanuni za ujenzi wa majengo, barabara na madaraja.
- Kutayarisha bajeti ya mwaka ya ujenzi na matengenezo ya barabara, madaraja na majengo.
- Kusimamia na kuratibu kazi za barabara/madaraja na majengo zinazofanyika katika Halmashauri.

## **2. Dereva Daraja II Nafasi 5**

### **Sifa za Mwombaji**

- Awe Mtanzania mwenye umri wa miaka 18 hadi 45,
- Cheti cha kidato cha nne (form IV).
- Leseni ya udereva daraja la E au C
- Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na chuo cha mafunzo ya ufundi stadi (VETA) au chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.
- Awe na cheti cha majaribio ya ufundi Daraja la II (Grade test II)
- Ngazi ya mshahara ni TGS B
- Maombi yaambatanishwe na picha mbili (2) passport size.
- Maombi yaambatanishwe na cheti cha kuzaliwa cha mwombaji.

## **Majukumu:**

- Kuendesha gari
- Kuhakikisha gari na vyombo vyake vipo katika hali nzuri wakati wote.
- Kufanya uchunguzi wa gari kabla na baada ya safari ili kugundua ubovu unaohitaji matengenezo.
- Kufanya matengenezo madogo madogo katika gari,
- Kutunza na kuandika daftari la safari log-book kwa safari zote.

Maombi yatumwe kwa,  
Mkurugenzi Mtendaji (W),

S .L. P 320,

**KYELA.**

Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe **10.11.2021** saa **9.30**  
**ALASIRI.**

Watakaokidhi vigezo na kuchaguliwa kwa ajili ya usaili watajulishwa.

Imetolewa na:-



**MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
KYELA**

**EZEKIEL H. MAGEHEMA  
MKURUGENZI MTENDAJI (W),  
HALMASHAURI YA WILAYA,  
KYELA**